
# Uniongoze ee Roho Mtakatifu

Eugène AMPIRE Bisimwa






Uniongoze ee Roho Mtakatifu,
Na mwanga wako uniangazie,
Nitembee njiani mwa uzima,
Nikiongozwa nawe daima milele.

1. Njoo Roho Mtakatifu,
Moyo wangu uujaze.
Unilinde Roho,
Niongozwe katika uwepo wako.

2. Njoo Roho wa rehema,
Moyo wangu uutakase.
Uniwezeshe Roho,
Nikuabudu kwa hofu na imani.

3. Njoo Roho wa hekima,
Nuru katika giza,
Fungua macho yangu,
Ili nione utukufu wa Mungu.

4. Njoo Roho wa mapendo,
Ndani mwangu uzidishe
Neema na fadhila,
Ya kutangaza mapendo ya Mungu.

5. Njoo Roho wa ibada,
Roho wa vipai tele.
Fanyiza kinywa changu
Kitangaze sifa zake Mwenyezi.